



Haki za muislamu juu ya muislamu mwenzake ni sita" Pakasemwa: Na ni zipi hizo ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?, akasema: "Ukikutana naye msalimie, na akikuita muitikie, na akikutaka nasaha mnasihi, na akipiga chafya akamhimidi Mwenyezi Mungu basi muombe dua ya rehema, na akiugua mtembelee, na akifariki msindikize

Imepokelewa kutoka kwa Abuu Huraira -radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-
yakwamba Mtume -rehema na amani ziwe juu yake- amesema: "Haki za muislamu juu
ya muislamu mwenzake ni sita" Pakasemwa: Na ni zipi hizo ewe Mjumbe wa Mwenyezi
Mungu?, akasema: "Ukikutana naye msalimie, na akikuita muitikie, na akikutaka nasaha
mnasihi, na akipiga chafya akamhimidi Mwenyezi Mungu basi muombe dua ya rehema,
na akiugua mtembelee, na akifariki msindikize".

[Sahihi] [Imepokelewa na Imamu Muslim]

Amebainisha Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuwa miongoni mwa haki za muislamu
juu ya ndugu yake muislamu ni mambo sita: La kwanza: Amsalimie akikutana naye kwa
kusema: Assalaam alaikum, naye atajibu salamu kwa kusema: Waalaikumussalaam. La pili:
Kuitika wito wake atakapomuita kwa ajili ya sherehe ya harusi au nyingineyo. La tatu: Kumpa
nasaha akizihitajia, na wala usimsifie bure, au kumfanyia udanganyifu. La nne: Akipiga
chafya akasema: Alhamdulillah, basi muombe dua kwa kusema: Yar-hamkallaah
(Akuhurumie Mwenyezi Mungu), naye ajibu kwa kusema: Yah-diikumullaahu wayuslih
baalakum (Akuongozeni Mwenyezi Mungu na kutengenezeeni hali zenu). La tano: Akamuone
na amtembelee atakapougua. La sita: Amswalie atakapofariki, na alisindikize jeneza lake
mpaka azikwe.

النجاة الخيرية
ALNAJAT CHARITY

